JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU KINAMPANDA

Anuani: Kinampanda T.C.
Simu: 0732 960850
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 532,
KINAMPANDA,
SINGIDA.

Kumb.No KCCU/PS/A/III/2014/100

20/08/2018

Ndugu……
……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA ASTASHAHADA YA UALIMU (ELIMU YA AWALI/MSINGI) MWAKA WA MASOMO 2017/18, MUDA WA KOZI NI MIAKA MIWILI (2)

* **UTANGULIZI**:
Napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na **Mafunzo ya AStashahada ya Ualimu *Elimu ya …….*** katika **Chuo cha Ualimu Kinampanda**.

Mafunzo tajwa yatakuwezesha kutumia mbinu mbalimbali zitakazowawezesha watoto/Wanafunzi wa ngazi hii kujifunza kwa ufanisi. Mwelekeo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni **kumwandaa mwalimu mahiri mwenye ujuzi stahiki katika Elimu ya Awali/Msingi**.

Aidha, mafunzo utakayopata yatakupatia sifa na ujuzi wa kufundisha hapa **Nchini** na **Nchi za nje** kwa kuzingatia fursa za soko la ajira ndani na nje ya Nchi. Elimu ya Awali/Msingi ni msingi mkuu katika utoaji wa Elimu na imepewa kipaumbele katika Sera ya Elimu na Mafunzo iliyoboreshwa mwaka 2014**. HONGERA SANA**.

Chuo kipo Mkoani Singida, Wilaya ya Iramba, umbali wa kilometa 65 toka mjini Singida, kufuata barabara iendayo Mwanza. Kutoka Singida utapanda mabasi yaendayo Kiomboi ambayo hupitia Kinampanda na ukitokea Mwanza utashuka njia-panda ya Kinampanda (Kitusha).

DIRA YA CHUO:
KUWA KITUO CHENYE MAZINGIRA BORA YA KUANDAA NA KUENDELEZA WALIMU KITAALUMA NA KITAALAMU KWA MAENDELEO ENDELEVU YA TAIFA LETU.

MOTTO WA CHUO: ELIMU NI KAZI.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(i) Kama umekubali kujiunga na kozi hii katika chuo hiki huna budi kuzingatia na kufuata kanuni na taratibu za mwenendo bora chuoni. Kuwa na heshima, nidhamu na maadili ya Ualimu.

(ii) Unatakiwa kutumia hekima na busara katika maamuzi yote utakayoyafanya ukiwa hapa chuoni.

* Simu za mkononi **haziruhusiwi** kutumika katika vyumba vya madarasa, mitihani, wakati wote wa masomo ya jioni (Prep), mikutanoni na katika shughuli zote rasmi za chuo. Ukibainika unatumia simu katika maeneo hayo utanyang'anywa, utapewa adhabu kali na utarudishiwa mwisho wa mafunzo.
* Kumbuka kujaza fomu iliyoambatanishwa ya kukiri kupokea maagizo ya kujiunga na chuo pia soma kanuni, sheria na taratibu zote za chuo kabla hujafika chuoni. Mzazi/mlezi ajaze sehemu yake, kisha ikabidhiwe ofisi ya usajili mara ufikapo chuoni.

* MASHARTI YA USAJILI

Ili uweze kusajiliwa unatakiwa utekeleze yafuatayo:

* Unatakiwa ulete cheti chako/vyeti vyako halisi (Original certificate/s) vya kufuzu mtihani wa kidato cha nne (Form IV)/sita(form VI) {CSEE/ ACSEE} au Result Slips kama cheti/vyeti havijatolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Vyeti vya kuhitimu Elimu ya Sekondari (leaving certificate).
* Ulete cheti halisi (Original certificate) cha kuzaliwa na nakala yake (Photocopy). Ikibainika kuwa umeleta vyeti vya kughushi au cha mtu mwingine utashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchi.
* Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **04/10/2018** usipofika hadi tarehe **18/10/2018** utakuwa umejikosesha nafasi hiyo mwenyewe.
* Usajili utafanywa katika Ofisi ya Msajili wa Chuo ambapo na vifaa vingine vitakaguliwa.
* Ni kosa kwa mwanachuo kutosajiliwa mara baada ya kufika katika eneo la Chuo.

* ADA NA MICHANGO:

(i) ADA:

Ada ya chuo ni Tshs. 600,000/= kwa mwaka au Tshs. 300, 000/= kwa muhula. Ilipwe kwenye akaunti ya Chuo **'Kinampanda Teachers' College', NMB Kiomboi Acc. No. 5061100010** NA UJE NA RISITI HALISI YA BENKI (Pay in Slip) sio nakala (Photo copy) yake. Usipoleta risiti hutapokelewa chuoni.

(ii) MICHANGO MINGINE

a. Michango yote hii ilipwe kupitia Akaunti ya Chuo '**Kinampanda College of National Education', NMB Kiomboi Acc. No. 5062300001** na uje na risiti halisi ya Benki (Bank Pay in Slip) zingatia na tofautisha akaunti ya Ada na Michango.
b. Ada ya mitihani ya NECTA ni Tshs. **50,000/= na 5,000/=** kwa ajili ya kutuma fedha NECTA**.** Fedha hiyo italipwa mwanzo wa mwaka wa mwisho wa mafunzo.
c. Fedha ya huduma ya kwanza ni **Tshs. 5,000/=** kwa mwaka.
d. Mwanachuo anashauriwa kuja na kadi ya Bima ya Afya kama anayo au aje na **Tshs. 50,400/=** kwa ajili ya bima ya afya ya Taifa.
e. Gharama ya kitambulisho ni **Tshs.10,000/=** na Usajili ni **Tshs.5,000/=** italipwa wakati wa kusajiliwa. Ukipoteza kitambulisho utalipia kutengenezewa kitambulisho kingine.
f. Usafi na miundombinu **Tshs. 20,000/=**
g. Mchango wa mahafali ya chuo **Tshs.10,000/=** kwa mwaka.
h. Godoro linakodishwa kwa **Tshs.20,000/=** kwa mwaka.
i. Mchango wa serikali ya wanachuo **Tshs. 5,000/=** kwa mwaka.
j. Mchango wa Ulinzi na Vibarua ni **Tsh.15,000/=** kwa mwaka.
k. Tahadhali **Tshs.20,000/=** kwa mwaka.
l. Michezo **Tshs10,000/=** kwa mwaka.
m. ICT/TEHAMA **Tshs 20000/=** kwa mwaka.
n. T-Shirt yenye **Tshs.15,000/=** kwa mwaka.
o. Taaluma **Tshs.50,000/=** kwa mwaka.

** Zingatia na tofautisha akaunti ya Ada na Michango mingine. Hakikisha "**Bank Pay in - slip**" imeandikwa *Ada kwa ajili ya* (**jina la mwanachuo**) au *Michango kwa ajili ya* (**jina la mwanachuo**)

* **VITU MUHIMU**

A: SARE YA CHUO

* **Wasichana**

  1. Sketi nyeusi mbili (2) ndefu hadi kuvuka magoti za mshono uliooneshwa hapa chini. (mchoro wake huu hapa)

* Shati Bluu bahari (Light Blue) mbili (2), mikono mirefu.
* Tai ndefu nyeusi **PANA.**
* Viatu vyeusi vya Ngozi vyenye kisigino kifupi na soksi nyeupe fupi. Sio "vibajaji".
* Wasichana wa Kiislamu wanatakiwa kuja na Hijabu za rangi ya Bluu Bahari (Light Blue) kwa ajili ya kuvaa wakati wa Vipindi.

* **Wavulana**

  1. Suruali nyeusi mbili (2) za kushonwa mshono wa kawaida sio Jeans. Kama inavyoonekana hapa chini.

  2. Shati Bluu Bahari (Light Blue) mbili (2) mikono mirefu.
  3. Tai ndefu nyeusi **PANA.**
  4. Viatu vyeusi vya Ngozi vyenye kisigino kifupi na soksi nyeusi za kawaida.
  5. Mkanda wa ngozi mweusi usio na urembo.

NB: Mwanachuo aje na Suti nyeusi.

B: SARE YA MICHEZO

(i) **Wasichana**:

1. Bukta ya Pinki na Sketi fupi ya rangi ya pinki.
2. Raba nyeupe na soksi nyeupe ndefu
3. Track-suit ya Bluu Bahari (Light blue)

(ii) **Wavulana**:

1. Bukta ya rangi ya Bluu
2. Raba nyeupe na soksi nyeupe ndefu
3. Track – suit ya bluu Bahari (Light blue).

C: VIFAA VINGINE MUHIMU:

* Daftari za kutosha (Counter book) na kalamu za kutosha unaweza kununua katika duka la chuo.
* Rimu moja (1) ya karatasi (Photocopy paper size A_4) **kwa kila muhula**.
* Mkebe wa Hisabati (Mathematical Instrument set) unaweza kununua katika duka la chuo.
* Shuka mbili (2) za rangi ya Bluu isiyo na maua (Plain Blue)
* Mto, Foronya ya rangi ya Bluu na Chandarua.
* Vyombo vya chakula vya udongo (Sahani, Bakuli, Kikombe) na Kijiko uje navyo.
* Ndoo ya kutunzia maji ya ujazo wa lita 20 na ya lita 10.
* Fagio la nje (chelewa mbili) na fagio la ndani (soft broom)

NB: Ada na michango ikishalipwa **hairudishwi** endapo mwanachuo ataacha, kuachishwa au kuahirisha mafunzo.

* AFYA YAKO:

Unapaswa kupimwa afya yako kwa Daktari wa Hospitali ya Serikali kabla ya kuripoti chuoni. Fomu imeambatanishwa. Mwenye afya duni inayohitaji chakula maalum (Special Diet) ni vyema asije chuoni kwani chuo hakitoi chakula hicho.

* WAGENI:

Mwanachuo haruhusiwi kutembelewa na mgeni yeyote kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, isipokuwa Jumamosi na Jumapili kuanzia saa 7.00 mchana hadi saa 10 jioni na siku za Sikukuu kuanzia saa 4.00 asubuhi hadi saa 10 jioni. Mgeni huyo awe ni Mzazi/Mlezi au Ndugu wa karibu wa mwanachuo na ajitambulishe kwa Uongozi wa Chuo kupitia Mkufunzi wa zamu/Waziri wa zamu katika ofisi ya zamu ndipo akutane na Mwanachuo husika. Hata hivyo chuo hakina nafasi ya kulaza wageni wa wanachuo chuoni, ila wageni wanaweza kutumia " Guest house " ya chuo na watalipia.

* MITIHANI:

Chuo hutoa mitihani, unatakiwa ufaulu mitihani yote unayopewa. Chuo hakitasita kukurudisha kama utashindwa kufaulu mitihani inayotolewa.

* KANUNI ZA CHUO

Kanuni za Chuo utakabidhiwa siku ya mafunzo kabilishi, ambazo utatakiwa uzisome kisha uzifuate na kuzizingatia wakati wote ukiwa mwanachuo. Kama utaona huwezi kuzitekeleza, NASHAURI USIJE .

10. MENGINEYO:

Shabaha ya Chuo :

KUANDAA MWALIMU BORA MWENYE ARI NA UWEZO WA KUFUNDISHA SHULE ZA MSINGI.

NB: NJOO NA BARUA HII YA MAELEKEZO, USIPOKUJA NAYO HUTAPOKELEWA.

Karibu Chuo cha Ualimu Kinampanda – Iramba – Singida.

MAULID H. NJAU
MKUU WA CHUO

KIAMBATISHO NA.2

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

TO: The Medical Officer From: Kinampanda Teachers' College
……..
……..

Please examine the above named as to his /her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a)Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious Diseases

B: blood group

Date:……
Signature……

Official Stamp

PART B: **MEDICAL CERTIFICATE.**
(To be completed by Government Officer)

I have examined the above named Student that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher Education course.

* (a) Eye – sight ……
* Hearing ……
* Limbs ……..
* Speech ……..
* Leprosy ……...

II. Neuroses ……
III. Other serious Diseases ……..
IV. Pregnancy ……..

Date: …… Signature: ……

FOMU YA KUKIRI

* **MWANACHUO**

Mimi ……(Majina rasmi) naishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kunipa nafasi ya kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya **Astashahada ya Elimu ya Awali/Msingi** katika Chuo cha Ualimu Kinampanda.

Nakiri kupokea maagizo ya kujiunga na chuo pia kanuni, sheria na taratibu zote za chuo. Baada ya kusoma na kutafakari kwa kina, naahidi kutekeleza yote niliyoagizwa na kufuata kanuni, sheria na taratibu zote wakati wote wa mafunzo chuoni. Na nitatekeleza wajibu wangu wote nikiwa mwanachuo kwa kusoma na kufanya kazi kwa bidii kwani ni kweli kwamba **ELIMU NI KAZI**.

Naahidi hayo mbele ya Mzazi/Mlezi wangu.

Sahihi ya Mwanachuo:……

Anwani:……..

Tarehe:……..

* **MZAZI/MLEZI**

Mimi Mzazi/ Mlezi wa …… nimesoma na kuelewa maelezo na kanuni , sheria na taratibu zote za chuo. Nipo tayari kushirikiana na chuo wakati wote wa mafunzo kuhusu Malezi ya mtoto wangu.

Jina la Mzazi/ Mlezi:……

Sahihi:……

Anwani: ……

Simu no: ……

Barua pepe: ……

Tarehe: ……..